**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MJI NEWALA**

Shule ya Sekondari Nambunga

S.L.P 131,

**NEWALA, MTWARA.**

**Tarehe ........................**

**MAWASILIANO.**

Mkuu Wa Shule: 0784553279

Makamu Mkuu wa Shule 0714583398/0783800936

Patron 0659525545

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ................................**
**S.L.P ..............................................................**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI NAMBUNGA HALMASHAURI YA MJI NEWALA MKOA MTWARA MWAKA...........**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka ............... na atasoma tahasusi ya **PCB/CBG.**
Shule ya Sekondari **Nambunga** ipo umbali wa **Kilometa 14** Kaskazini mwa Mji wa Newala barabara ya kuelekea Mji wa Masasi. Usafiri wa basi kutoka mjini Newala unapatikana katika kituo cha mabasi cha Newala na nauli ni Shilingi **2,000**. Na kwa pikipiki ni shilingi **6000** hadi **8,000**.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe............ hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe............ Mwisho wa kuripoti ni tarehe................**.**

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 (a) Sare za Shule

Mwanafunzi aje na sare zifuatazo:

i) Suruali mbili (2) dark grey (Tumia kitambaa grade 1) zenye upana nchi 7.5 chini, mifuko mitatu,

ii) Mashati mawili (2) meupe tetroni ya mikono mirefu, aje nayo

iii) Tai mbili (2) ndefu rangi hiyo ya suruali.

iv) Sweta mbili (2) za maroon (damu ya mzee).

v) Viatu jozi mbili rangi nyeusi vyenye visigino vifupi.

vi) Soksi nyeusi jozi mbili.

vii) T-shirt mbili rangi ya light blue zisizo na mandishi mengi au zisizo na rangi mchanganyiko.

viii) Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi.

ix) Suruali mbili nyeusi za kushindia (shamba dress) upana nchi (7.5) na mifuko mitatu.

X). T-shirt zenye nembo ya Shule za rangi ya damu ya mzee (Maruni) iwapo mzazi hataweza kuzipata huko aliko basi anaweza zipata kwenye maduka yaliyo Jirani na shule kwa bei ya Tshs 20,000/= (Elfu ishirini).

### 2.1 (b) Sare za michezo

i. Traki suti ya rangi nyeusi moja.

ii. Bukta mbili rangi ya light blue

iii. Fulana mbili light blue zisizo na maandishi (jezi)

iv. Stocking /soksi rangi ya light blue

v. Raba jozi moja

(Sare zote hizo za michezo anapaswa kuja nazo)

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni

i. Madaftari makubwa (counter books Quire four) yawe tisa (9) na madaftari ya msomi 15 kwa ajili ya mazoezi

ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;

iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika PCB na CBG

iv. Dissecting Kit na dissecting tray kwa wanafunzi wanaosoma somo la Biology;

v. Scientific Calculator;

vi. Godoro dogo size 2.5 x 6

vii. shuka mbili rangi ya light blue 2, blanket 1, foronya ya godoro 1 , foronya ya rangi ya light blue, mto wa kulalia, chandarua 1 rangi nyeupe, taulo moja

viii. Nguo za ndani za kutosha;

ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
x. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
xi Kwanja 1, jembe 1, reki 1, fagio 2 za ndani na mmoja wa nje.
Xii Result slip (kivuli) ya kidato cha nne.
Xiii File / jalada la kutunzia kumbukumbu za mwanafunzi
Xiv Dawa ya chooni lita 5 Lita 2.5 kwa muhula mmoja
Xv Picha za passport size nne (04).
Xvi Graph paper pads ream mbili (2)

**2.3 Michango mbalimbali**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**MALIPO YALIPWE KWENYE AKAUNTI YA SHULE YA BENKI YA NMB**
- ✓ **JINA LA AKAUNTI YA BENKI *NAMBUNGA SECONDARY SCHOOL***
- ✓ **NAMBA YA AKAUNTI *70801200065.***

**WANAFUNZI WAJE SHULENI NA KADI ZA BIMA YA AFYA KWA AJILI YA MATIBABU NA KWA WALE WASIO NA BIMA YA AFYA WAJE NA FEDHA TSHS 50,400/= (Elfu hamsini na mia nne).**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Night Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;

v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;

- Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;

- Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kufuga ndevu;
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
x. Kusababisha mimba;
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;

xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xiv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KWA NIABA YA WANAJUMUIYA YA SHULE YA SEKONDARI NAMBUNGA**
**NINAKUKARIBISHA SHULENI HAPA**
**KARIBU SANA**

**MKUU WA SHULE**

**NB:** Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. **TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**THE PRIME MINISTER'S OFFICE REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

Nambunga Secondary school,
P. O. Box 131,
**NEWALA.**

Medical Officer.

………………………………

**STUDENT'S FORM FOR MEDICAL EXAMINATION**

To be completed by Medical Officer in respect of all students joining in our school.

Student's full name…………………………………………………………

- Age ………. …….Year ……….. Sex ………
- Blood count (red and White) ……..
- Urine …………….
- Stool ……………….
- Venereal Disease …………
- T. B ……………….
- Ears ………………
- Eyes ………….
- Spleen ………….
- Chest …………

**ADDITIONAL INFORMATION**

If any, Eg Physical defects

Arm or leg impairments, chronic or family diseases

Etc

I certify that she / he is fit / unfit to pursue advanced secondary education as stated.

Signature …………………….. Station ……………..

Designation …………………. .Date …………

## TAARIFA BINAFSI KWA MWANAFUNZI

**SEHEMU A**

Jina kamili (kwa herufi kubwa) ............................................................

Tarehe ya kuzaliwa ............................................................................

Jina la baba / mama / mlezi ..............................................................

Kazi yake ...... Namba ya simu ................. Anuani ya nyumbani........Barua pepe ........... Kijiji ...............Kata .............. Tarafa .................... Wilaya ............. Mkoa ...................... Kabila ................. Dini ................

Uraia ........................

Mambo unayopendelea kufanya nje ya masomo (kwa mfano: michezo, Bustani na kuchora)

1............................................ 2...................................... .........
3.............................................. 4................................................

**SEHEMU C**

MICHANGO ITALIPWA NA ..................................................................

**SEHEMU D**

Ninaahidi kuwa na tabia nzuri na mwenye bidii katika masomo yangu. Nimesoma maelezo yote na kuzielewa sheria za shule, Mungu nisaidie.

Sahihi ya mwanafunzi ....................... Sahihi ya mzazi / mlezi.................

Tarehe .................... Tarehe ...........................

**FOMU YA MAKUBALIANO NA MZAZI / MLEZI**

Mimi ........................................................... ambae ni mzazi / mlezi wa ...............................................................

***(nakubali au sikubali masharti yafuatayo) kata neno mja.***

1. Nafasi aliyopewa kijana wangu kujiunga na kidato cha tano kwa mwaka wa masomo ...........
2. Kijana wangu kufuata sheria, maagizo na masharti yote ya shule ya sekondari Nambunga.
3. Kulipa michango yote itakayoelekezwa na shule.
4. Kumpatia mwanangu mahitajii yote ya shule kama yalivyoorodheshwa na shule.
5. Kufuatilia kwa karibu maendeleo ya kila siku ya mwanangu tabia, mwenendo na taaluma
6. Kupokea taarifa zote kutoka shuleni zinazomuhusu mwanangu na kuzifanyia kazi kwa wakati.

Ahsante

JINA.................................................. SAHIHI...................... TAREHE...................

**MKATABA WA KUTOJIHUSISHA NA VURUGU, MGOMO FUJO NA MAKOSA YA JINAI**

*(Fomu hii ijazwe na kurudishwa shuleni)*

Mimi ………………………………………………………………ambaye ni mwanafunzi

wa kidato cha ………… katika shule hii naahidi kutojihusisha kwa namna yoyote katika migomo, fujo au kosa lolote la jinai ambalo litahatarisha amani au litakalokuwa kinyume cha sheria, kanuni na taratibu za shule.

Endapo ikithibitika kuwa nimetenda kosa au makosa tajwa hapo juu sitakuwa na pingamizi juu ya hatua za kinidhamu zitakazochukuliwa dhidi yangu:

Jina la mwanafunzi ……………………………………………

Sahihi ya mwanafunzi ………………………………………

Tarehe…………………………….

Jina la mzazi / mlezi …………………………………………

Sahihi ya mzazi / mlezi …………………………

Tarehe ………………………………..